

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA KILIMO NA  
WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA

NYONGEZA NA. 1 YA MWONGOZO NA.1 WA USIMAMIZI WA  
MASOKO NA MAUZO YA KOROSHO GHAFI WA MWAKA  
2022/2023

TOLEO LA PILI

BODI YA KOROSHO TANZANIA  
TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA  
BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA



A handwritten signature in black ink.

A handwritten signature in black ink.

A handwritten signature in blue ink.

**NYONGEZA NA. 1 YA MWONGOZO NA. 1 WA USIMAMIZI WA MASOKO NA**  
**MAUZO YA KOROSHO GHAFI WA MWAKA 2022/2023**

**KWA KUWA,** mnamo tarehe 22 Septemba 2022 Bodi ya Korosho Tanzania, Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala walipitisha Mwongozo Na. 1 wa Usimamizi wa Masoko na Mauzo ya Korosho kwa msimu wa Mwaka 2022/23 (Mwongozo);

**KWA KUWA,** mnamo tarehe 10 Oktoba 2022 Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) na Shirika la Bima la Taifa (NIC) walisaini makubaliano (MoU) kuhusu utoaji wa kinga ya utendaji katika ghala (performance bond);

**KWA KUWA,** Makubaliano kati ya NIC na WRRB yanalenga kurahisisha taratibu za malipo kwa Wanunuzi endapo kutatokea upungufu wa korosho ghafi wakati wa kutoa mzigo katika ghala kutokana na sababu ambazo zitathibitishwa na Bodi kuwa hazijatokana na Mwendesha ghala;

**KWA KUWA,** Serikali imeridhia maoni ya wadau kuwa utaratibu wa uendeshaji wa minada ubadilike ili zabuni za ununuzi wa korosho ghafi zipokelewe na kufunguliwa siku ya mnada badala ya utaratibu wa awali ambapo zabuni zilikuwa zinawasilishwa siku moja kabla ya siku ya mnada; NA

**KWA KUWA,** Wadau wote wameridhia utaratibu wa malipo kutokana na upungufu wa korosho ghafi na utaratibu wa uendeshaji wa minada uwekwe katika Mwongozo; hivyo imelazimu kufanya marekebisho katika Mwongozo Na.1.

**HIVYO BASI** Nyongeza hii inashuhudia yafuatayo:

1. Kwamba, Nyongeza hii itasomwa pamoja na Mwongozo Na. 1 kama ulivyosainiwa tarehe 22 Oktoba 2022.
2. Kwamba, Kifungu cha 3.2.10 kinarekebishwa na kitasomeka kama ifuatavyo:

"Mwendesha Ghala/Mnunuzi watatakiwa kuzingatia masharti ikiwa ni pamoja na kujaza Fomu Namba 7 ndani ya siku 3 tangu kubainika kwa tatizo la upungufu wa mzigo ghalani au tatizo lolote kuhusu uzingatiaji wa masharti ya viwango au

1 ABayoh

uhifadhi na utoaji wa korosho ghalani". Utaratibu wa kufidla upungufu utakuwa kama ifuatavyo:

- i. Mwendesha Ghala na Mnunuzi watatakiwa kusaini Fomu Namba 7 kwa pamoja na kuiwasilisha Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala ndani ya siku 3 tangu kubalnika kwa tatizo la upungufu wa mzigo ghalani. Jukumu la kuwasilisha fomu husika linaweza kutekelezwa na Mwendesha Ghala au Mnunuzi.
  - ii. Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala itafanya uhakiki wa fomu husika ndani ya siku 3 na kuiwasilisha kampuni ya NIC kwa ajili ya malipo kwa Mnunuzi.
  - iii. Kiwango kitakachobebwa na Kinga hii kitazingatia utendaji wa Mwendesha ghala na alama anazopata wakati wa ukaguzi.
  - iv. Kampuni ya NIC itafanya malipo kwa Mnunuzi ndani ya siku 4 baada ya kupokea nyaraka zote muhimu kutoka WRRB kwa kiwango kilichoelekezwa na Bodi.
  - v. Iwapo mwendesha ghala atapatikana na mapungufu wakati wa utendaji wake basi mapungufu hayo yatagharimiwa na Mwendesha ghala kwa kurejesha fedha zilizolipwa na Kampuni ya NIC kwa uwiano.
3. Kifungu namba 4.1.3 kinarekebishwa na kitasomeka kama ifuatavyo:  
"Maombi ya zabuni za ununuzi wa korosho yatapokelewa katika sanduku la zabuni yakiwa yamefungwa kwa lakiri (seal) siku ya mnada kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana na kufunguliwa mbele ya wakulima kwenye vituo vya mnada vilivyoainishwa kwenye ratiba".
4. Kwamba, Nyongeza hii itaanza kutekelezwa mara baada ya kusainiwa na wahusika.


5. Kwamba, vifungu vya Mwongozo Na. 1 ambavyo havijafanyiwa marekebisho na Nyongeza hii vitaendelea kusomeka na kutekelezwa kama vilivyo.

Nyongeza hii imetolewa na kusainiwa leo tarehe ..... Oktoba 2022.



**Francis Alfred**

Kaimu Mkurugenzi Mkuu - Bodi ya Korosho Tanzania



**Dk. Benson O. Ndeige**

Mrajis wa Vyama vya Ushirika - Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania



**Asangye N. Bangu**

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji - Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala